# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

**17 MEI, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 17 MEI, 2022

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**207. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Mangopacha Nne ili kuwanusuru Akinamama wajawazito.

**208. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti magari yanayopakua na kupakia mizigo Kariakoo, Mtaa wa Msimbazi na barabara ya Morogoro.

## WIZARA YA MAJI:

**209. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mradi wa maji safi na salama katika Kata ya Rabour.

## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**210. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Posta katika Wilaya ya Micheweni.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**211. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali haioni haja ya kurekebisha utaratibu wa kuwaachia makusanyo ya fedha Jeshi la Uhifadhi hasa TANAPA.

**212. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kwa nini Serikali isitumie mbao za Mitikiti zenye ubora sawa na Mninga/Mkongo kwani tenda za Serikali zinataka Mninga/Mkongo.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**213. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha kuvuja kwa mitihani nchini.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**214. MHESHIMIWA RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN (CHAKECHAKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Askari wa Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kusini Pemba.

**215. MHESHIMIWA HAJI MAKAME MLENGE (CHWAKA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza msongamano wa Watu wanaofuatilia Hati za kusafiria.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA KILIMO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**17 MEI, 2022**
**DODOMA**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**